5. Ni kwa njia gani tutaupata upendo huu? Warumi 5: 5.
6. Je! Ni jambo gani pekee yake tumeshauriwa kuwa na deni kwa mtu yoyote? Warumi 13: 8 (sehemu ya kwanza).
7. Ni nini tunafanya wakati tunapopendana? Mstari wa 8 (sehemu ya mwisho).
8. Je! Bwana wetu alisisitizaje ukweli huu? Mathayo 22: 34-40.
9. Tunawezaje kuthibitisha upendo wetu kwa kila mmoja? Wagalatia 5: 14, 15.

   **Maelezo**: Katika upendo wetu kwa Elohim, na mwanadamu mwenzetu, ndiyo utimilifu wa sheria zote na manabii. Ikiwa tunamdhuru ndugu yetu kwa njia ya kueneza uvumi ni dhahiri kwamba upendo ambao Elohim aliweka ndani ya mioyo yetu umepungua kwa kiasi fulani, kwa maana upendo haufanyi vibaya kwa jirani yake.
10. Je! Yahshua alisisitizaje upendo wake mkuu kwetu? Yohana 15:13.
11. Bwana ametuamuru aje sisi kupendana? Aya 12.
12. Je! Upendo huu utasababisha sisi kuvaa nini? Wakolosai 3:12.

*******************************



mkate, akaubariki na akasema, chukua mle huu ni mwili wangu. Mkate huu usiochachwa uliwakilisha Mwili Wake. Kumla kondoo wa Pasaka sasa ilikuwa mambo yaliyokwisha milele. Pasaka ilikuwa historia. Yahshua alikuwa akianzisha Chakula cha jioni cha Bwana.

8. Baada ya kula mkate usiotiwa chachu, Yahshua alifanya nini? Luka 22:20; Mat. 26:27.
9. Je, Yahshua alisema kinywaji kilichokuwa katika kikombe kiliwakilishwa nini? Marko 14:24; Mat. 26:28; Luka 22:20. Linganisha na Yohana 6:53, 54.
10. Je, kikombe ambacho Yahshua aliwapa wanafunzi wake kilikuwa na nini? Marko 14:25; Mat. 26:29.

    **Maelezo**. - Injili za Mtakatifu Marko, Mtakatifu Luka na Mtakatifu Mathayo, hutuambia kwamba kikombe ambacho Yahshua alibariki kilikuwa na matunda ya mzabibu. Hii ilikuwa damu safi ya zabibu, ambayo inawakilisha damu ya thamani ya Yahshua. Tafadhali angalia Kumbukumbu 32:14, sehemu ya mwisho. Elewa kwamba kilichomo ndani ya kikombe hiki hakikuwa na divai iliyochachuka, wala maji, lakini ni damu ya zabibu, matunda ya mzabibu.
11. Je, ni sawa katika maandiko kwa kuita chakula cha jioni cha Bwana kama ushirika? 1 Wakor. 10:16.



9. Ni kwa nini Masihi hangepokea heshima ya wanadamu wakati alikuwa duniani? Yohana 5: 40-44.
10. Ni katika njia gani Mwokozi alipata heshima kubwa? Phil. 2: 7-11.
11. Kwa nini alijitwalia hali duni ya umaskini? 2 Wakor. 8: 9.
12. Ni wapi hazina zetu zinapaswa kuhifadhiwa? Mat. 6:20, 21.

******************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Pili
2024

Ya
Aprili, Mei, Juni.
**(Adar II, Nisan, Iyar, Sivan)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

**Maelezo**. - Paulo akiandikia kanisa la Elohim huko Korintho kuhusu Chakula cha jioni cha Bwana ambacho Yahshua alianzisha wakati walipokuwa wakila Pasaka, kabla ya kuhukumiwa kwa ukatili alikiita Chakula cha jioni cha Bwana, au ushirika.

12. Je, Yuda alikuwapo na alishiriki katika chakula cha jioni cha Bwana? Luka 22:21; Yohana 13:18.
13. Je, kila mtu anapaswa kufanya nini kabla ya kula chakula cha jioni cha Bwana? Ikiwa tutashindwa, matokeo ya kusikitisha yatakuwa yapi? 1 Wakor. 11: 27-30.

*******************************

**Somo la Aprili 27, 2024 [Nisan 19, 5784]**

## MATESO YA YAHSHUA

**Somo Kuu: Isaya 53:1-12.**
**Fungu la Kukariri: 1 Timotheo 1:15.**

1. Je! Kwa nini Masihi alikuja ulimwenguni? 1 Tim. 1:15.
2. Je! Ni nini kilichomsukuma Elohim kuruhusu Mwana wake mwenyewe afe kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi? 1 Yohana 4:9, 10; Warumi. 5:8.
3. Je! Nabii alisema Masihi ataitwa kuvumilia nini? Isaya 53:7, 8 .



7. Ni swali gani la kutafakari Yahshua aliuliza Petro? Yohana 21:15.
8. Jinsi gani Petro alihisi wakati Bwana alimuuliza mara ya tatu kama kweli alimpenda? Yohana 21:17.
9. Wakati Petro aliona mwanafunzi ambaye Bwana alimpenda akimfuata, ni jambo gani alimuuliza Bwana? Yohana 21:20, 21.

*******************************

**Somo la Juni 8, 2024 [Sivan 2, 5784]**

## UPENDO KATI YA MMOJA NA MWINGINE

**Somo Kuu: Yohana 14: 15-31.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 14:21.**

1. Je! Moja ya sifa za Elohim ni gani? 1 Yohana 4: 8, 16.
2. Jinsi gani Elohim alidhihirisha upendo wake kwa ulimwengu? Yohana 3:16; Warumi 5: 8; Waefeso 2: 4,5.
3. Ni nini kinachohitajika kwa kila mtu anayekubali Masihi kama Mwokozi wake? Yohana 13:34; 15: 9, 10, 12.
4. Je! Dunia itawezaje kujua kwamba sisi ni wafuasi wa Masihi Yahshua? Yohana 13:35.



**Somo la Aprili 6, 2024 [Adar II 27, 5784]**

## KUCHUKULIWA MIMBA NA KUZALIWA KWA YAHSHUA

**Somo Kuu: Mathayo 1: 16-25.**
**Fungu La Kukariri Mathayo 1:18.**

1. Je! Malaika alimpa Mariamu ujumbe upi? Luka 1: 28-31.
2. Je, Mariamu alishangaa na kile ambacho malaika alimwambia? Luka 1:34; Matayo.1:18.

   **Maelezo**. Maandiko Matakatifu yanatuambia kwamba Mariamu alikuwa bikira aliye safi sana kwamba hakujua mtu. Alikubali kuolewa na Yusufu, lakini kabla ya kumjua kama mkewe, alipata mtoto kwa njia ya Roho Mtakatifu. Matayo.1: 18-20; Luka 1:35.
3. Je! Ni uhusiano gani ulikuwa kati ya Yusufu na Mariamu kabla ya kuzaliwa kwa Yahshua? Ni nini ambacho kilikuwa chanzo cha mimba ya Masihi? Matayo.1:18; Luka 1:35.
4. Je! Isaya alitabiri nini juu ya tukio hili la ajabu? Isa.7:14; linganisha na Matayo.1:23; Luka 1:31.
5. Je! Yusufu alitaka kufanya nini? Matayo.1:19.
6. Ni nini malaika wa Bwana alimwambia Yusufu katika ndoto? Matayo.1: 18-25.
7. Wakati Yusufu na Mariamu walipofika Bethlehemu walipokelewa aje? Luka 2: 4-8.



huathiriwa. Ni mabadiliko kutoka kwa dhambi na kuingia katika utakatifu, ni tukio la ajabu kuzaliwa tena katika familia ya Elohim.

*****************************

**Somo la Juni 29, 2024 [Sivan 23, 5784]**

## AHADI KWA WANYENYEKEVU

**Somo Kuu: 1 Petro 5: 1-11.**
**Fungu La Kukariri: 1 Petro 5: 6.**

1. Je! Petro alitoa mawaidha gani ya busara? 1 Petro 5: 5.
2. Je! Ni agizo gani linaloambatana na ahadi ambalo Petro pia alitoa? Mstari wa 6.
3. Je! Tunawezaje kudhibitisha kuwa tunastahili kuitwa na Yeye? Efe. 5: 1, 2.
4. Je! Ni zawadi gani ambayo ni muhimu kwa wokovu Elohim huwapa wanyenyekevu? Mit. 3:34; Yakobo 4: 6.
5. Anaahidi kukaa na kuhuisha nani? Isa. 57:15.
6. Je! Ni matokeo gani tofauti kwa wale wanaonyenyekea, na wale wanaojiinua? Mat 23:12; Mit. 29:23.
7. Ni nini iko katika Mithali 15:33 ambayo inathibitishwa katika Esta 7: 9, 10, 9: 1-5?
8. Je! Baraka za kidunia zinaambatana na unyenyekevu? Mit. 23: 4, 5.

tunapokuwa naye pekee yetu. Ingawa ni kweli kabisa ya kwamba tunabarikiwa sana na uwepo wake katika nyakati hizo, pia ni kweli ya kwamba, mara nyingi kuliko itupasavyo, tunaye kando katika benchi ya kazi, katika ofisi, wakati sisi tunaosha vyombo, kuendesha gari au shughuli yoyote ya kila siku tunayoshiriki. Hizo ni nyakati ambazo tunaweza kosa kumtarajia, na isiwe hivyo. Kazi yetu lazima iwe ya kupendeza kwa Bwana, ili kazi yetu iweze kubarikiwa naye.

**Somo Kuu: Marko 16:9-20**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15:16.**

1. Ni amri gani Yahshua aliwapa wanafunzi wake kuhusu kuhubiri neno? Marko 16:16; Mathayo 28: 19; Matendo 1: 8.
2. Kabla ya Bwana Yahshua hajapaa kwenda mbinguni, ni wapi wanafunzi wake walikuwa wamekusanyika? Yohana 21:2, 3.
3. Ni nini inathibitisha kwamba Bwana hakupendezwa na kile walichokuwa wakifanya? Yohana 21:3, sehemu ya mwisho.
4. Ni nani ambaye alionekana ufuoni? Yohana 21:4.
5. Nini kilitendeka wakati walitii amri ya Bwana? Yohana 21:6.
6. Inawezekana kwetu kutimiza chochote bila yeye? Yohana 15:5.



4. Je, Masihi alijua mbeleni jinsi ambavyo angechukiwa na kudharauliwa, na hatimaye kusulubiwa? Luka 18:31-33.
5. Yahshua alijua yote yatakayompata, na jinsi angeteseka na kusulubiwa. Je! Alikuwa tayari kwa kiasi gani kupitia haya yote ya aibu na mateso? Luka 22:41, 42; Mt. 16:21-23; 26:37-39.
6. Je, uchungu wa nafsi Yake ulikuwa mkubwa kiasi gani na ni nini kilitokea kumsababishia huzuni zaidi? Luka 22:44, 47, 48 .
7. Ni kitendo gani cha Petro kilisababisha Mwokozi kuteseka zaidi? Luka 22:59-6l.
8. Ni mambo gani ya laumu ambayo Yahshua alitendewa kwenye nyumba ya kuhani mkuu? Luka 22:63, 64 .
9. Pilato alimtendea Yahshua ukatili gani? Yohana 19:1.
10. Je! Ni mateso gani ya aibu aliyopata kutoka kwa askari? Mt. 27:29, 30, 41, 42 .
11. Je! Ni maombi gani ya ajabu aliyoyatoa kwa ajili ya watesi wake alipokuwa akining'inia msalabani? Luka 23:34.
12. Je, ilikuwa ni lazima kwa Masihi kuteseka na kufa? Waebrania. 2:10.
13. Kuona jinsi Masihi alivyoruhusiwa kuteseka haya yote kwa ajili yetu, hii ni changamoto gani kwa wafuasi wake? Warumi 8:31,32.

*******************************



6. Ni nini sababu nyingine iliyoelezwa na Neno, kwamba ubatizo wa maji ni muhimu? Wakolosai 3: 1, 2, 5, 9; Matendo 22:16.

   **Maelezo**. – Kuamka kutoka kwenye kaburi la maji la ubatizo ni tendo muhimu ambalo inayohitajika ili uwe kiumbe kipya katika Masihi Yahshua, kwa kuwa kila aliyezaliwa tena anazaliwa upya, anazaliwa na operesheni ya Elohim. Maisha mapya ni muhimu, si tu kuenenda katika upya wa uzima (Warumi 6: 4) bali hata kuwa na mawazo sawa ya Ufalme wa Elohim.
7. Mtume Paulo alisema ubatizo unatufanyia nini? 1 Pet. 3:21.
8. Jinsi gani damu ya Yahshua inaweza kututakasa dhambi zote na kutuondolea aibu? 1 Wakor. 6:11.

   **Maelezo**. "Kuzaliwa tena ni mwanzo wa maisha mapya. Maisha mapya ya kujitahidi kuwa mkamilifu katika Masihi Yahshua. Wakati utu wa kale umeondolewa sio mabadiliko ya kimsingi hutendeka; mtu aliyebadilika bado hufikiri, hutoa hoja, hutamani, hupenda, hukumbuka na hufanya kazi. Lakini mawazo yake makuu, ya upendo, ya chuki, hubadilishwa; na kuwa mapya. Ni mabadiliko makubwa zaidi ambayo tabia ya binadamu



8. Ni jina gani alilopewa mtoto na malaika hata kabla hajazaliwa? Matayo.1:25.
9. Je, umuhimu wa jina hili umesisitizwa aje? Matendo 4: 10-12: Wafilipi. 2: 9-11.
10. Je, Paulo alisema nini kuhusu utimilifu wa hili? 1 Tim.3:16.

    **Maelezo**. Unabii huu na utimilifu wake umekuwa lengo la wasioamini na watu wa kisasa kwa karne nyingi. Hapa nguvu ya Elohim ilidhihirishwa na mimba ya kimiujiza na kuzaliwa kwa Mwana wake mpendwa, Yahshua. Mara kwa mara, Yahshua aliwambia wasikilizaji wake kwamba alikuja kutoka juu na kwamba Elohim alikuwa Baba Wake.
11. Je! Ni nini kilichotokea wakati wachungaji walikuwa wakilinda kondoo zao? Luka 2: 8-14.
12. Walipata tukio gani na malaika? Je! Hii ilikuwa na athari gani? Luka 2: 9.
13. Je! Ni ishara gani waliyopewa kuhusu mtoto huyu? Luke 2:12.
14. Je! Ni eneo gani lenye utukufu ambalo wachungaji waliruhusiwa kushuhudia? Luka 2: 13-14.
15. Jinsi gani malaika walionyesha furaha yao kwa wakati huo, ni nini kilichofanyika? Luka 2:14.
16. Wachungaji wa kondoo waliitikiaje tangazo hili? Luka 2: 16-20. Je, hii inafaa kuwa mfano kwetu sisi? Isaya 12.

*****************************

### Somo la Mei 4, 2024 [Nisan 26, 5784]

# MAANA YA KIFO NA KUFUFUKA KWAKE YAHSHUA KWETU SISI

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 15:1-23**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 15:22, 23.**

1. Je, ni sababu gani Isaya alitoa kwa ajili ya unabii wa kifo cha Masihi? Isaya 53: 8.
2. Je, Kifo cha Masihi Mwana, kiliamriwa na Elohim Baba? Isaya 53: 6, 10.
3. Je, mwana wa Elohim alijitolea, au alilazimishwa kufa? Mathayo 26:53; Yohana 10:17, 18.
4. Je, Masihi alitabiri kifo na kufufuka kwake mwenyewe? Mathayo 20:18, 19, 16:21-23.
5. Je, baadaye Masihi alikuwa nani? Waebrania 5:8, 9.
6. Jinsi gani tunafaa kukumbuka kifo cha Yahshua? 1 Wakorintho 11:26-32.
7. Yahshua alitabiri nini kuhusu kufufuka kwake? Yohana 2:19-22; Marko 9:31.
8. Kwa nini maisha, kifo na kufufuka kwa Masihi Yahshua, mwana wa Elohim, kulikuwa kwa muhimu? (a) ili kutimiza maandiko: Luka 24:44-46; (b) kwa ajili ya msamaha wa dhambi:1 Wakorintho 15:17; (c) kwa ajili ya kuhesabiwa haki: Warumi 4:25; (d) ili kufanya maombezi: Warumi 8:34; Waebrania 9:24.



5. Je! Kulikuwa na mapatano na umoja wa nia na moyo katikati yao? Matendo 4:32; 2:46.
6. Je! Mitume walikuwa na nia gani kuhusu msiba na ustawi wa ndugu zao? Waefeso 1: 15-19.
7. Walitesekaje kwa sababu ya Yahshua na Injili? Waebrania 11: 36-38.
8. Walikuwa wakarimu kiasi gani? Matendo 2:45; 4:32.
9. Je! Tabia ya maisha yao kwa roho ambazo zilivutwa kwa Bwana kupitia kwa mahubiri yao ilikuwa ipi? 1 Wathesalonike 2: 2; 5: 7-10.
10. Je! Walikuwa na maoni gani kuhusu mateso na dhiki kwa wale waliowatesa? Matendo 5: 40,41; 2 Wakorintho 12:10.
11. Je! Mathiya alihesabiwaje na mitume kumi na mmoja? Ilikuwa ni kwa upendeleo, uteuzi, ukoo, uchaguzi wa kura au **"casting of lot"**? Matendo 1: 23-26.
12. Walichukuliaje ushirika wa pamoja wa ndugu? Matendo 2: 42-46.

*****************************

### Somo la Juni 1, 2024 [Iyar 24, 5784]

# YAHSHUA AWATOKELEZEA WANAFUNZI WAKE BILA KUTARAJIWA

Yahshua yu nasi kila siku. Hatupaswi kumtafuta siku ya Sabato tu, katika mikutano ya maombi au nyakati za kimya



### Somo la Aprili 13, 2024 [Nisan 5, 5784]

# USHAHIDI KATIKA MAANDIKO KWAMBA MASIHI NI MWANA WA ELOHIM

**Maelezo.** Kuna maandiko zaidi ya 250 katika Agano la Kale yalitimizwa katika matukio ya kuzaliwa, maisha, kifo na ufufuo wa Yahshua ambaye ni Masihi. Mbali na nguvu zake za ajabu katika kuponya wagonjwa na kufufua wafu, Yahshua alitimiza unabii wote kuhusu Masihi Myahudi aliyeahidiwa.

**Somo Kuu: 1 Kor. 15: 1-9; Yohana 5: 38-47.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 5:46**

1. Ni sehemu gani ya maandiko ambayo imerejelewa katika Yohana 5:38?
2. Je! Paulo alitangaza kwamba Mwokozi wetu alikuja kulingana na Agano la Kale? 1 Wakor. 15: 3,4
3. Je! Masihi, ambaye Wayahudi wanasubiri leo, kuja kama mtawala mwenye nguvu, au alikuwa akuje kama mwana? Isa. 7:14, 16; 9: 6,7; 11: 1.

   **Maelezo.** Ishara ilikuwa kwamba bikira angeweza kuchukua mimba na kuzaa mtoto huyu, na pia kwamba nchi ingekuwa imekwisha kunyimwa wafalme wote wawili kabla ya yeye kuwa na umri



10. Katika uchambuzi wa mwisho, tutakuwa tunafanya nini? 1 Yohana 3:24.

*****************************

### Somo la Juni 22, 2024 [Sivan 16, 5784]

# KUVUA UTU WA KALE – KUVAA UTU UPYA

**Somo Kuu: Warumi 6.**
**Fungu La Kukariri: Wakolosai 3: 9.**

1. Mtu anapotubu na kukubali ukombozi kupitia Masihi Yahshua Bwana wetu, anafaa kufanya nini? Matendo 2: 37-41.

   **Maelezo**. - Ubatizo huu wa maji ulitolewa kwa watu waliotubu na kujiimarisha katika Masihi Yahshua, na kukataa dhambi za ulimwengu huu.
2. Ubatizo unamaanisha nini, na hutimiza nini kwa wote wanaojinyenyekeza na wanaomtii Yeye aliyemwita mtu kuja kwake? Warumi 6: 3
3. Je! MMasihi hufanya tendo gani, na ni nini MMasihi huacha wakati alipoamini, akabatizwa katika Masihi Yahshua? Warumi 6: 1, 3, 4-8.
4. Je, kuzaliwa upya na ubatizo wa maji ni muhimu ili kuingia katika ufalme wa Elohim? Yohana 3: 5-7.
5. Mtume mkuu Paulo anaelezeaje jambo hili? Wakol. 2:11, 12.

14. Kwa msingi wa ufunuo huu [na kukiri kwa Petro], Yahshua alisema nini kwa Petro? Alimhakikishia nini? Mathayo 16:18.
15. Tulipewa faraja kubwa katika uwakilishi wa kiroho wa Funguo za Ufalme. Je! Utumiaji wa funguo hizi utatufaaje? Mathayo 16:19.

*******************************

**Somo la Mei 25, 2024 [Iyar 17, 5784]**

## MAISHA YA MITUME

**Somo Kuu: Matendo 2.**
**Fungu La Kukariri: Matendo 2:42.**

1. Je! Mtume Petro alisema kuwa wafuasi wa Bwana wanapaswa kutumia mfano wa nani? 1 Petro 2:21; 1 Yohana 2: 6; Waefeso 5: 1.
2. Katika kufuata nyayo za Yahshua, jinsi gani mitume wa Yahshua walikuwa na bidii na shauku; katika kufuata wito wa mbinguni? Mathayo 4: 18-22; Marko 10:28.
3. Baada ya kuacha shughuli zao za kibinafsi (kazi) kwa sababu ya Injili, Je, wengine wao walikuwa watumishi na viongozi wakuu wa serikali za nchi yao walitendaje? Luka 5: 27-32; Wafilipi 3: 7,8; Luka 19: 1-8.
4. Ni kwa njia gani wanafunzi hawa wa Yahshua waliojitolea walipata riziki yao? 1 Wakorintho 4:12; Matendo 18: 3.



9. Ni matendo gani yanaashiria kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Masihi? Warumi 6:3-6.
10. Jinsi gani Masihi alijidhihirisha kwa Yohana katika kisiwa cha Patimo? Ufunuo 1:17, 18.

*******************************

**Somo la Mei 11, 2024 [Iyar 3, 5784]**

## WAO WALIO WA MASIHI WAMESULUBISHA MWILI

**Somo Kuu: Warumi 6: 1-18.**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 5:24.**

1. Mwanzoni mwa Warumi 6, je! Paulo anaanzisha mada mpya, au anaendeleza mada ya sura iliyopita? Je! Unafikiri Paulo na wainjilisti wengine wanapaswa kudumu sana kuhusu somo hili?
2. Katika kuhubiri Injili ya Ufalme, je! Paulo alisisitiza juu ya mada hii, au zaidi juu ya neema, upendo, nk? Warumi 6:23.
3. Unafikiria ni nini maana ya kichwa cha somo hili? Tazama Wagalatia 5:24; Wakolosai 3: 5-9 na wengine wengi.
4. Kulingana na Warumi 6: 3, 4, ubatizo unaashiria nini?
5. Sasa, ikiwa tumekufa pamoja na Masihi katika kaburi lenye maji, je, tumewekwa huru kutoka kwa laana ya Adamu? Warumi 6: 6, 7.



**Maelezo**: Moffatt hueleza jambo hili: “Kila mtu anayeamini kwamba Yahshua ndiye Masihi amezaliwa na Elohim; na kila mtu ambaye hupenda Baba hupenda wana waliozaliwa naye. Hivi ndivyo tuna uhakika kwamba twawapenda watoto wa Elohim, kwa kumpenda Elohim na kutii amri zake.”

4. Jambo ili limesemwa vipi mahali pengine? Yohana 13:34, 35.

**Maelezo**: Kinyume cha hoja ambayo Masihi alitumia katika mstari wa 35, haitaonekana ya kwamba, kama upendo wa kidugu hautakuwepo baina yetu, hatutakuwa wanafunzi wake?

5. Je, ni nini hutimiza sheria? Warumi 13:1-13.
6. Jinsi gani ni lazima tujitenganishe na ulimwengu kabisa? Yohana 17:14.
7. Wakati tutajisalimisha kwa Elohim kwa ukamilifu, mwenendo wetu utakuwa upi? 1 Yohana3:9.
8. Jinsi gani tutaweza kuyafanya maisha yetu ya uMasihi kuvutia zaidi na yenye faida? 2 Wakorintho 6:14.

**Maelezo**: Hii bila shaka inajumuisha swali la ndoa lakini si hilo tu. WaMasihi wengi wamekwazika sana katika kazi yao ya kuhubiri, na pia katika utunzaji wa Sabato kwa sababu ya “kufungiwa pamoja isivyofaa” katika biashara.

9. Jinsi gani ingine maisha yetu yataonyesha kwamba sisi tumezaliwa tena? Wagalatia 5:24-26.



wa kutosha wa kujua mema na mabaya. Herode alikufa (Mathayo 2:14, 15) na Archelaus akatawala mahali pake na pia yeye akatolewa, kabla ya Masihi kuwa na umri wa miaka sita kulingana na maelezo yote ya kihistoria.

4. Alikuwa azaliwe wapi? Mika 5: 2; Mathayo. 2: 1-5.
5. Je, Yahshua Masihi alipaswa kukatiliwa mbali na kuuwawa, au alikuwa aurejeshe ufalme? Dan. 9:26 (sehemu ya kwanza).
6. Nini kilichotokea Yerusalemu baada ya kukatiliwa mbali kwake? Mji ulikusudiwa kuwa ukiwa? Dan. 9:26 (sehemu ya mwisho.)

**Maelezo.** Ikiwa kuja mara ya kwanza kwa Masihi bado ni wakati ujao, basi Yerusalemu itaharibiwa tena na nchi Takatifu kuwa ukiwa. Ukweli wa uharibifu wa Yerusalemu tayari ulitokea (wakati Mkuu wa Kirumi Tito, aliharibu mji mwaka wa 70 A.D) ina maana kwamba, kulingana na unabii, Masihi alishakuja.

7. Masihi alikuwa ahesabiwe na wahalifu na kuzikwa pamoja na matajiri. Je! Hii ilitimizwa katika kifo cha Masihi? Marko 15:27, 28; Mat. 27: 57-60.
8. Ni unabii upi mwingine, uliotimizwa wakati wa kusulubiwa kwake? Mat. 27: 34-36. Linganisha na Zaburi 22:17, 18.

*******************************

6. Je! Unafikiri mateso ya mwili yaliyotajwa katika 1 Petro 4: 1, 2 yanahusu maumivu ya mwili? Eleza.
7. Injili ingewezaje kuhubiriwa kwa wafu kama ilivyoonyeshwa katika 1 Petro 4: 6 na mtu anawezaje kubatizwa kwa ajili ya wafu kama ilivyoelezwa katika 1 Wakorintho 15:29?
8. Je, kufa kwa dhambi na vitu vyote katika maisha haya kutatufaidi katika maisha yajayo? Fikiria Warumi 6: 8-11.
9. Je! Ni ushauri gani wa ajabu Paulo anaoutoa katika Warumi 6:12, 13?
10. Kwa nini alitoa mawaidha haya? Warumi 6:14, 15.

*******************************

**Somo la Mei 18, 2024 [Iyar 10, 5784]**

## CHACHU YA WAFARISAYO

**Somo Kuu: Mathayo 16: 1-20.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 16:17.**

1. Je! Ni makundi gani mawili yaliyomjia Yahshua? Kusudi lao lilikuwa nini katika kuuliza ishara? Mathayo 16: 1.
2. Je! Yahshua alitoa jibu gani? Je! Tunaweza kujifunza nini kutokana na jinsi alivyojibu? Mathayo 16: 2,3.



3. Ni kwa maneno gani Yahshua alionyesha hali ya mioyo yao? Je! Ni ishara gani pekee yake wangepata? Mathayo 16: 4.

   **Maelezo**: Ishara na miujiza ambayo Mwokozi wetu alifanya, haikuvutia mawazo yao ya kimwili. Walitaka kitu cha kushangaza, kitu cha kuonyesha asili ya mwanadamu. Yahshua hakuweza kuwaridhisha katika hili, lakini aliwaonyesha ishara ya Yona [pia katika Mathayo 12:40.]

4. Je! Wanafunzi waligundua nini wakati huu? Mathayo 16: 5.
5. Je! Bwana aliwapa onyo gani? Mathayo 16: 6.
6. Jinsi gani wanafunzi walitafsiri onyo hili? Mathayo 16: 7.
7. Katika kuwakosoa kwa ukosefu wa imani yao, aliwakumbusha nini? Mathayo 16: 8-11.
8. Baada ya Yahshua kusema, wanafunzi waligundua nini? Mathayo 16:12.
9. Je! Yahshua aliuliza swali gani lenye uzito kwa wanafunzi wake huko Filipi? Mathayo 16:13.
10. Alipata majibu mangapi? Yalikuwa yapi? Mathayo 16:14.
11. Je! Alitaka kwao jibu gani la moja kwa moja? Mathayo 16:15.
12. Je! Petro alitoa uthibitisho gani? Mathayo 16:16.
13. Mwokozi alilichukulia jibu hili kwa njia gani? Mwandishi wa ufunuo huu alikuwa ni nani? Mathayo 16:17.



**Somo la Aprili 20, 2024 [Nisan 12, 5784]**

## MWILI WANGU NI CHAKULA CHA KWELI, NA DAMU YANGU NI KINYWAJI CHA KWELI

**Somo Kuu: Yohana 6: 22-71.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 6:54.**

1. Je, Yahshua alienda wapi baada ya kulisha watu elfu tano? Yohana 6: 24-25.
2. Ni kwa nini umati mkubwa ulimtafuta Yahshua? Yohana 6:26.
3. Yahshua aliwaambia nini kuhusu chakula? Alisema chakula hiki kinaweza kupatikana kutoka wapi? Yohana 6:27.
4. Je! Inaonekana kwamba umati huu ulifikiria kuwa ulikuwa na mkate huu kutoka Mbinguni? Jinsi gani Yahshua aliwajibu? Yohana 6: 31-35.
5. Je,Wayahudi walilichukuliaje neno hili ambalo Yahshua alinena? Yohana 6:42.
6. Yahshua alijibu aje manung’unika yao? Yohana 6:48, 50, 51, 53-58.
7. Wakati Yahshua alianzisha chakula cha jioni cha Bwana, alisema mkate usiotiwa chachu uliashiria nini? Luka 22:19 Mat. 26:26. Linganisha na Yohana Mtakatifu 6:51, 53.

   **Maelezo**. - Wakati Yahshua na wanafunzi wake walipokuwa wakila Pasaka, Yahshua alichukua



**Somo la Juni 15, 2024 [Sivan 9, 5784]**

## UTHIBITISHO WA KUZALIWA UPYA

**Somo Kuu: 1 Yohana 3**
**Fungu La Kukariri: 1 Yohana 4:7, 8.**

1. Ni nini kilichosemwa kuhusu WaMasihi wa Korintho kwamba ni kweli kwetu sisi wakati huu wa sasa? 2 Wakorintho 3:2.
   **Maelezo**: UMasihi katika hali yake ya kweli hauwezi kufichika kwa mtazamo. Ni ukweli sawia kwamba ukosefu wa UMasihi hauwezi kufichwa na muumini mwanaume au mwanamke. Sisi hatufai kutajwa tu kama WaMasihi, ni lazima tujitahidi kuwa kama jinsi hilo jina linamaanisha.
2. Ni kwa kanuni gani iliyo ya kale sisi huwa bado twapimwa nayo? Mathayo 7:20.

   **Maelezo**: Hii ni kuhusu mstari mmoja tu baadhi ya wakosoaji wa Biblia huonekana wamejifunza. Hata hivyo ni kweli kwamba tunapaswa kuzalisha matunda kwa ajili ya utukufu wake. Ni jambo baya sana kuweka madai kwa jina la mtu mwingine na kujaribu kuendelea na tabia ya huyo mtu.
3. Je, ni mambo yapi mawili yanayothibitisha mtu amezaliwa upya? 1 Yohana 5:1-3.